
# SIKU ILE NILIYOKUITA

Wilbert M. Olomi
Sinon, Arusha
July, 2019






Tuni nyingine



1. Nitakushukuru kwa moyo wangu wote/
   Mbele ya miungu nitakuimbia zaburi,
   nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu.

2. Nitalishukuru jina lako,
   kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako,
   kuliko jina lako lote/
   siku ile niliyokuita uliniitikia,
   ukanifariji nafsi kwa kunitia nguvu.

3. Ingawa Bwana yuko juu amwona mnyenyekevu,
   naye amjua mwenye kujivuna tokea mbali/
   nijapokwenda katika shida utanihuisha,
   utanyosha mkono juu ya hasira ya adui zangu.

4. Na mkono wako wa kuume utaniokoa,
   Bwana atanitimiliza mambo yangu/
   Ee Bwana fadhili zako ni za milele,
   usiziache kazi za mikono yako.